**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA**

# SHULE YA SEKONDARI UKENYENGE

**S.L.P 84 KISHAPU**

**SHINYANGA, TANZANIA.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule 0785804594 / 0626870621/0759304574**

**Makamu Mkuu wa Shule 0744310332 / 0628573760**

**Shule ya Sekondari UKENYENGE.**

**S.L.P. 84 KISHAPU**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………..**

**S.L.P ……………………**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI UKENYENGE HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU MKOA WA SHINYANGA**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii na atasoma tahasusi ya Chemistry, Biology, Geography**(CBG)**

Shule ya Sekondari UKENYENGE ipo umbali wa Kilometa 25 kutoka njia panda ya Kolandoto kuelekea Mashariki na kilometa 22 kutoka Kishapu (Mhunze) kuelekea Magharibi mwa Mji wa KISHAPU. Usafiri wa kutoka kolandoto/Mhunze unapatikana katika kituo cha mabasi Nauli ni Shilingi 4,000/= Basi.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ................, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe ………………….. ( zingatia maelekezo ya tarehe yaliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI.)

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni suruali mbili rangi ya kahawia iliyoiva (brown) (*mbili*). Maelezo ya mshono, iwe na marinda mawili kila upande,isiwe ya kubana/iwe na pindo au turnup kwa chini ba upana usipungue inchi 17-18.***Wasiliana na uongozi wa shule kabla hujashona kama maelezo ya kitambaa hujayaelewa****.*

ii. Suruali Moja rangi ya kijivu-kwa ajili ya Kushindia, iwe na marinda mawili kila upande na isiwe ya kubana.

iii. Mashati **meupe** (*mawili, mikono mirefu*);.

iv. Sare ya Michezo ni **trucksuit 1**, **T-shirt** 1, **bukta 1**(zote *rangi ya Blue)*

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

vi. Soksi **jozi mbili** nyeupe ndefu za shule;

vii. Sweta mikono mirefu (*rangi ya kahawia,* ***moja*** ) ;

viii. Tai (rangi ya kahawia *mistari myeupe, moja(01)*;

Viii.Tisheti (T-shirt) **Kijivu** yenye kola na nembo ya shule*, (moja*)

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari Nane (08) (*counter books 3 or 4 quires*);

ii. **Ream (A4) ya** Karatasi –**DOUBLE A**, Mbili (2) kwa mwaka;(ream 1 kila mhula)

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha ambatishwa*);

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

v. Scientific Calculator kwa wanafunzi wa science, geography, Maths

vi. Godoro **futi 3.5**,

*vii.* Mashuka 2 ya rangi ya blue, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 Nyeupe pembe nne .

viii. Nguo za ndani za kutosha;

ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. **VIFAA VYA USAFI:** Jembe,Sabuni ya Maji lita 01, Soft bloom, Squizer na Reki.
xii. Taulo.

**NB. Kwa mzazi/mlezi atakayependa sare na baadhi ya mahitaji yanapatikana Shuleni kwa gharama ya Shati mbili-25,000/=, Tshirt-15,000/=, Sweta-15,000/=,Truck Suit-20,000/=,Bukta-5,000/=,Godoro-(Malaika-45,000/=, superbanco-60,000/=),Shuka mbili-24,000/=, Neti-10,000/=, file-2000/=**

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Malipo yote haya yafanyike benki NMB, Akaunti namba 30701100069- Jina la akaunti UKENYENGE SEKONDARI.**
**Mtumaji Andika jina la mwanafunzi na afike na payslip siku ya kuripoti.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi anapaswa kuheshimu dini na imani za wengine.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote hawaruhusiwi kusuka na hivyo kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI UKENYENGE**

**Saini ya Mkuu wa Shule …………………**

**Jina la Mkuu wa Shule …………………………………….**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0785804594 au 0626870621 au 0759304574**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0744310332 au 0628573760**
- **Mwandamizi Malezi 0757441331 au 0658854752**

**-Mzazi anashauriwa kumkatia BIMA ya Afya mwanao,**

## MEDICAL CERTIFICATE FORM

**To be completed by a Government Medical Officer in respect of:-**

Pupil's full name: …………………………………………………..

Blood count (Red and White): ………………………………………

Stool Examination: ………………………………………………….

Analysis: …………………………………………………………….

Syphilis Test: ………………………………………………………..

Eye Test: …………………………………………………………….

Ears: …………………………………………………………………

Chest: ………………………………………………………………..

Spleen: ………………………………………………………………

Abdomen: ……………………………………………………………

Pregnance test (for girls)UPT……………………………………….

ADDITIONAL INFORMATION: E.g Physical defects or impairments infections, chronic or family disease that needs special attention (if any)

……………………………………………………………

I certify that the above is fit/ unfit for admission into a boarding secondary school

Signature: …………………………………………

Designation: ………………………………………

Station: …………………………………………...

Date: ……………………………………………..

Kiambatanisho No. 1

**MAELEZO BAYANA (IJAZWE NA MZAZI/ MLEZI)**

1. Jina kamili la mwanafunzi: ……………………………………………….
2. Tarehe ya kuzaliwa: ………………………………………………….
3. Jina la baba/ mlezi: ……………………………………………………...
4. Jina la mama: …………………………………………………….......
5. Kazi afanyayo baba: ………………………………………………………
6. Kazi afanyayo mama: ………………………………………………………
7. Anuani ya baba/ mama: ……………………………………………………
8. Mwanafunzi ana kilema chochote? ……………………………………………
9. Anapendelea kushiriki michezo gani? ………………………………………

Taja ndugu wanne (**4**) wa karibu wanaoweza kutoa msaada wakati mzazi anapokosekana muda mwanafunzi awapo shuleni. Picha zao (passport size) ziambatanishwe.

| **S/N** | **JINA LA MZAZI/ NDUGU** | **KAZI AFANYAYO** | **NAMBA ZA SIMU** |
|---|---|---|---|
| **1.** | | | |
| **2.** | | | |
| **3.** | | | |
| **4.** | | | |

**FOMU YA KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA ULIPAJI WA ADA**
**SEHEMU A: MWANAFUNZI**

Mimi …………………………………………… ninakiri kuzisoma sheria, kanuni, na taratibu zote za shule hii na ninakubali kuzitekeleza katika kipindi chote nitakapokuwa mwanafunzi wa shule ya sekondari Ukenyenge. Na endapo nitakwenda kinyume cha taratibu zilizopo, hatua kali za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu ikiwemo kufukuzwa shule kulingana na uzito wa kosa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Sahihi (isiyo ya kukoroga): ……………………………simu ya baba……………………..

Simu ya mama……………………..Tarehe: ……………………

NB: 1. ***Endapo mwanafunzi ataonekana dhaifu katika tahasusi aliyochaguliwa, atashauriwa kubadili tahasusi kulingana na ufaulu wake kidato cha nne.***

***2.Ni lazima kufika wanafunzi wote tarehe ya kufungua kila baada ya likizo na si vinginevyo***.

**SEHEMU B: MZAZI/ MLEZI**

Mimi mzazi/ mlezi wa mwanafunzi …………………………………………..ninakiri kukubaliana na sheria, kanuni, na taratibu za shule. Pia nikiwa kama mzazi/ mlezi wa mwanafunzi husika; ninakiri kukubali kumlipia ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule bila kusita wala kuichelewesha.

Jina la mzazi/ mlezi: …………………………………………..

Sahihi: ……………………………………………………………

Tarehe: …………………………………………………………..

Kiambatanisho No.2

**ORODHA YA VITABU**

| S/N | SOMO | JINA LA KITABU |
|---|---|---|
| | | |
| 1 | GEOGRAPHY | An Integrated Regional study on Human and Economic Geog |
| | | Africa in Diagram, By Bunnet |
| 2 | ADVANCED MATHS | Pure Mathematics 1 & 2 |
| | | Chand class XI, XII Vol. 1 &2 |
| | | Conceptual Advanced Mathematics |
| | | |
| 3 | CHEMISTRY | A-Level Chemistry, Ramsden |
| | | Organic Chemistry part 1, 2 |
| | | Inorganic Chemistry for A-Level part 1,2 |
| | | Soil Chemistry |
| | | Physical Chemistry A Level |
| | | CHAND XI, XII |
| | | |
| 4 | BIOLOGY | Biological Science |
| | | Comprehensive Biology |
| | | Understanding Biology |
| | | |
| 5 | GENERAL STUDIES | General studies for Advanced level |
| | | |